**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI MHESHIMIWA ESTHER NICOLOUS MATIKO (MB) KATIKA WIZARA YA MALIASILI NA UTALII KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

*(Inatolewa chini ya Kanuni 99(9) ya Kanuni za Bunge Toleo la mwaka 2016)*

Ofisi ya Bunge,
S. L. P 941,
**DODOMA**

Mei, 2017.

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema kusimama mbele ya Bunge lako tukufu kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Wizara hii muhimu. Aidha, napenda kutoa pole kwa Bunge lako kwa kuondokewa na wapendwa wetu Marehemu Samwel John Sitta aliyekuwa Spika wa Bunge la Tisa , Marehemu Hafidhi Ali Tahir aliyekuwa Mbunge wa Dimani na Marehemu Dr. Elly Marco Macha aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum.

**Mheshimiwa Spika,** Kipekee kabisa napenda kutoa shukrani zangu za pekee kwa familia yangu kwa upendo wao mkubwa wanaonionyesha. Napenda kuwaambia kuwa wao ni faraja kubwa katika maisha yangu na kila siku ninawaombea kwa Mwenyezi Mungu ili aendelee kuwapa ulinzi. Pia, nawashukuru sana wapiga kura wangu wa Tarime mjini kwa ushirikiano wao na upendo wanaonionyesha. Bado nitazidi kuwatumikia ndani na nje ya Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, napenda pia kutumia fursa hii kumshukuru Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni Mheshimiwa Freeman Aikael Mbowe (Mb) kwa kuendelea kuwa imara hata pale alipopata misukosuko ambayo mahasimu waliamini ingemrudisha nyuma katika kupigania demokrasia nchini.Vilevile, nitoe pongezi kwa viongozi wa UKAWA hususani kwa viongozi wa Chama cha Wananchi CUF kwa kuendelea kuwa wamoja hata pale ambapo imeonekana kuna baadhi ya watu wanataka kuwayumbisha kwa maslahi yao binafsi.

**Mheshimiwa Spika,** zaidi nimshukuru Naibu Waziri Kivuli wa Wizara hii Mheshimiwa Cecilia Daniel Pareso kwa kazi nzuri aliyoifanya na kutoa

ushirikiano katika kutekeleza majukumu ya kuandaa hotuba hii. Nitoe pongezi kwa Wabunge wenzangu wa Upinzani kwa kuendelea kuwa wavumilivu, wenye busara na zaidi kuendelea kuwa na umoja na mshikamano katika kutekeleza wajibu wao wa kuishauri serikali. Nipende kuwatia moyo tu kwa kutumia maneno haya kutoka kwa Obrien anasema **“ I’ve learned that fear limits you and your vision. It serves as blinders to what may be just a few steps down the road for you.The journey is valuabe, but believing in your talents, your abilities, and your self-worth can empower you to walk down an even brighter path. Transform fear into freedom-how great it that?”**Kwa tafsiri isiyo rasmi, *nimejifunza kwamba woga ni kikwazo kwangu na kwa maono yangu. Ni kama upofu kwa kile kilicho hatua chache tu mbele yangu. Safari hii ni ya thamani, amini katika kipaji chako, uwezo wako na thamani yako itakusaidia katika njia iliyo nyoofu .Geuza hofu yako kuwa ukombozi wako.*

**Mheshimiwa Spika**, baada ya utangulizi huu sasa naomba kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwenye Wizara hii ya Maliasili na Utalii kwa kuanza na nukuu ya Theodore Roosevelt kuhususiana na utatuzi wa matatizo ya uhifadhi wa maliasili zetu alisema”***The conservation of natural resources is the fundamental problem.Unless we solve that problem it will avail us little to solve all others”.***

## 2. 0 MASUALA MTAMBUKA KATIKA SEKTA YA UTALII NCHINI

### 2.1 HALI YA SEKTA YA UTALII NCHINI

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikitamani kuona sekta ya maliasili na utalii ikiwa ni moja ya sekta

ambazo huchangia mapato mengi ya nchi na pia kuchangia katika kuboresha huduma mbalimbali za kijamii. Hata hivyo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kuonesha masikitiko yake kutokana na kupungua kwa kasi ya ukuaji wa sekta hii tofauti na matamanio yake.

**Mheshimiwa Spika,** ni dhahiri kuwa kuna matatizo makubwa katika sekta ya utalii. Japokuwa takwimu zinaonyesha kuwa sekta hii inakuwa kwa takribani asilimia 11 tangu mwaka 2015-2016 kama ilivyoelezwa na Wizara kupitia kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii. Pamoja na takwimu hizo, ni ukweli usiopingika kuwa sekta ya utalii inaporomoka kwa kasi sana.

**Mheshimiwa Spika,** tafiti na habari kutoka katika vyanzo mbalimbali zinaonyesha kuwa wafanyabiashara wengi wenye hoteli za kitalii wamefunga hoteli zao kutokana na kupungua kwa watalii na hivyo kukosa wateja. Kuna kampuni mengi ya Utali ambayo tayari yamepunguza wafanyakazi kutokana na kupungua kwa idadi ya watalii nchini.

**Mheshimiwa Spika,**vilevile Wageni wanaokuja nchini kupitia makampuni makubwa ya kigeni ambapo wateja wake ni wale wenye uwezo mkubwa kifedha wamepungua, na hata hivyo,wale wanaokuja wanakimbilia katika hoteli zenye bei ya nafuu kutokana na kuongezeka kwa gharama za utalii nchini jambo ambalo limezua malalamiko mengi kutoka kwa wadau.

**Mheshimiwa Spika**, katika ripoti ya Wizara ya mwaka 2016 ilionyesha kuwa Idadi ya watalii wa kimataifa kwa mwaka 2015 ilikuwa ni Watalii 504,711 ikilinganishwa na mwaka 2016 ambapo idadi ya ilikuwa watalii 519,582 waliingia nchini. Takwimu hizi ni kinyume na takwimu zilizotolewa katika randama iliyowasilishwa kwenye kamati ya ardhi,

maliasili na utalii fungu 69 ambapo idadi ya watalii wa kimataifa waliotembelea nchini mwaka 2016 inaonekana kuwa ni watalii 1,284,279 ikilinganishwa na watalii 1,137,182 mwaka 2015. Takwimu hizi pia ni tofauti na ile yiliyotolewa kwenye randama ya Wizara fungu 69 ukurasa wa pili kwa mwaka 2015.

**Mheshimiwa Spika,** mkanganyiko huu wa takwimu ni ushahidi tosha kuna walakini katika kauli zinazotolewa kuhusu idadi ya watalii wanaotembelea nchi yetu. Pamoja na hilo, kuongezeka kwa fedha za kigeni kutoka dola 1,901.9 mwaka 2015 mpaka dola 2,073 mwaka 2016 inaweza kuwa sio sababu ya kuongezeka kwa watalii pekee kama ambavyo serikali inaamini. Ongezeko hilo la fedha za kigeni katika sekta ya utalii inaweza kuchangiwa pia na idadi ya siku ambazo wageni hukaa hapa nchini na aina za huduma au bidhaa wanazonunua wakiwa nchini.

**Mheshimiwa Spika**, tutambue kuwa sio kila mgeni aliyeorodheshwa uhamiaji ni mtalii. Maana halisi ya mtalii ***ni mtu yoyote anayesafiri au kutembelea eneo fulani kwa sababu za burudani au mapumziko (a person who is travelling or visiting a place for pleasure)***.Hii ni kwa mujibu maana halisi ya utalii kimataifa. Wapo wageni wengi wanaoingia nchini kwa shughuli mbalimbali zikiwemo za uwekezaji, biashara na shughuli mbalimbali za kijamii. Pamoja na hayo, serikali itambue kuwa tumefikia katika hatua mbaya ya kichumi na hivyo ni lazima kuboresha sekta hizi nyeti za kiuchumi ili kujinasua. Kuna msemo usemao ***"the deaf believe there is nothing wrong but the hearing believe something needs to be fixed"*** ikiwa na maana kwamba kiziwi haoni tatizo, ila anayesikia anaamini kuna jambo ambalo haliko sawa na linahitaji ufumbuzi.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kama sehemu mbadala ya serikali, inaona tatizo kubwa katika takwimu za ukuaji wa sekta ya utalii kama nilivyoonesha japokuwa serikali inaona kuwa sekta hii inakwenda vizuri. Sababu kubwa ni kuwa akili zinazotengeneza matatizo katika taifa haziwezi kamwe kuwa sehemu ya kutafuta suluhisho. Hivyo, Kambi Rasmi ya upinzani inaitaka serikali kufanya upya tathimini ya ukuaji wa sekta ya utaii badala ya kuonyesha wingi wa takwimu usio na tija kwani kufanya hivyo, hakusaidii ukuaji wa sekta hii.

## 2.2 MGOGORO SUGU WA LOLIONDO

**Mheshimiwa Spika**, mgogoro wa Loliondo ni mgogoro uliodumu kwa takribani miaka 30 sasa. Ni mgogoro uliogharimu maisha ya Watanzania wengi kutoka katika jamii ya wafugaji waishio katika bonde la Loliondo. Mgogoro huo umechochewa na pande tatu zinazosigana ikiwa ni upande wa wawekezaji, serikali na wananchi wanaoishi katika eneo hilo.

### Historia ya mgogoro wa Loliondo

**Mheshimiwa Spika**, Miaka ya 1980 mpaka 1993 Mfalme kutoka nchi za kiarabu alikuja Tanzania yeye na familia yake kwa shughuli za uwindaji wa wanyamapori. Mwaka 1992, walipokuja nchini walifanya uwindaji mkubwa zaidi ambao haukuwahi kutokea. Katika jarida la New York Times la tarehe 13 Novemba, 1993 liliandika kushtushwa na uwindaji huo wa kutisha wa wanyama kama Duma na Mbwa Mwitu ambao wapo katika hatari ya kutoweka.Vilevile gazeti la Mfanyakazi la tarehe 20,Januari 1993 lilichapishwa likiwa na kichwa cha habari "*Tanzania inavyoliwa na Waarabu*"

**Mheshimiwa Spika,** Mfalme na familia yake kupitia kampuni ya Otterlo Business Corporation Ltd (OBC) walipewa kibali cha uwindaji cha miaka kumi na aliyekuwa Waziri wa Utalii wa wakati huo Abubakar Mgumia kinyume na Sheria za wanyama pori namba 12 ya mwaka 1974, na Sheria ya Mashirika ya Umma namba 17 ya mwaka 1969 ambayo iliyataka makampuni binafsi walete wageni nchini kupitia shirika la Umma la wakati huo ambalo ni Tanzania Wildlife Corporation (TAWICO).

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na masharti hayo ya kisheria, kampuni hii ilipewa mkataba wa kumiliki ardhi ya vijiji sita vilivyo ndani ya hifadhi ya Loliondo. Mkataba huo uliotiwa saini na Marehemu Richard Koillah Punye aliyekuwa Mbunge pamoja na aliyekuwa Waziri wa Maliasili na Utalii Abubakar Mgumia. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona kuwa Mkataba huo uliwekwa saini kinyume cha Sheria kama nilivyoeleza.

**Mheshimiwa Spika**, Kitendo cha kampuni ya Otterlo kumilikishwa ardhi kilichochea kuongezeka kwa mgogoro kati ya kampuni hiyo na wananchi, ambapo wananchi wengi walichomewa maboma na walinzi wa kampuni hiyo mwaka 2000. Kufuatia hali hiyo vijiji vilivyoathirika na uchomoja wa makazi yao viliamua kuunda kamati ya wajumbe 13 waliotumwa kuonana na aliyekuwa Mheshimiwa Rais wa wakati huo Jijini Dar es Salam. Japokuwa hawakufanikiwa kuonana nae walikutana na mwandishi Jenerali Ulimwengu.

**Mheshimiwa Spika**, katika madai ya wanakijiji hao walizungumzia ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu uliofanywa na mwekezaji huyo, uharibifu wa mazingira, ukiukwaji wa haki za wanyama na kujenga majengo makubwa ndani ya hifadhi na karibu kabisa na mto

Olasai ambapo ni kinyume cha sheria za uhifadhi. Majengo hayo yaliyojengwa wakati huo mpaka sasa yapo na serikali haijachukua hatua yoyote pamoja na kujengwa kinyume na utaratibu.

**Mheshimiwa Spika**, Hata hivyo aliyekuwa Waziri wa Maaliasili na Utalii Bi. Zakiah Meghji alitoka hadharani na kuwapinga vikali wajumbe hao kupitia habari iliyochapishwa tarehe 11April, 2000 kwenye gazeti la The Guardian.

**Mheshimiwa Spika,** Desemba, 2005 mwekezaji huyo aliongezewa vijiji vingine viwili na kufanya jumla ya idadi ya vijiji nane ambavyo alipewa kumiliki ardhi yake katika shughuli za uwindaji. Hii ni kwa mujibu wa barua namba DC/NGOR/C.15/5/120 iliyoandikwa na aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Ngorongoro ndugu Jowika Kasunga.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na kuongezeka kwa mgogoro kati ya mwekezaji na wananchi ambao uligharimu maisha ya wananchi wengi na mifugo yao, mwaka 2009 aliyekuwa Mbunge wa Ngorongoro Ndugu Kaika Telele aliamua kuleta jambo hilo ndani ya Bunge (rejea hansard ya tarehe 11,Julai 2009). Pamoja na Mbunge huyo kuzungumzia sana mgogoro huo mpaka sasa hakuna suluhu iliyopatikana.

**Mheshimiwa Spika**, Mwaka 2010, aliyekuwa Spika wa Bunge, aliamuru kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuunda tume kwenda kuchunguza mgogoro huu wakati huo lakini pia haikuweza kuwa muarobaini wa mgogoro huu. Hata hivyo, aliyekuwa Waziri Mkuu wa wakati huo aliunda kamati ya Mawaziri sita akiwemo aliyekuwa Waziri wa Utalii kulifuatilia suala hilo mnamo tarehe 08 Februari 2010, kwenye kikao cha ndani cha Chama cha Mapinduzi. Kamati ile nayo haikuzaa

matunda na mpaka leo serikali hii ya awamu ya tano haijaweza kuwa muarobaini wa mgogoro huu.

**Mheshimiwa Spika**, ni hivi majuzi tu mwezi Februari 2017, Waziri Mkuu alimuagiza Mkuu wa Mkoa wa Arusha kufuatilia mgogoro huu ambao umedumu kwa muda mrefu. Timu hii ya Mkuu wa Mkoa imetumia mamilioni ya shilingi kama ilivyo kwa timu na Tume nyingine nyingi zilizopita katika kufuatilia mgogoro huu. Timu hii ya Mkuu wa Mkoa wa Arusha iliwasilisha mapendekezo yake ambapo wakati huohuo Waziri wa Maliasili na Utalii tayari alikuwa amekwisha kufanya maamuzi juu ya mgogoro huu ambapo alitoa kauli ya kutenga eneo la kilometa za mraba 4,000 kwa ajili ya pori tengefu la Loliondo na kuamuru eneo la kilometa 2,500 zilizokuwa zimechukuliwa na wawekezaji zirejeshwe kwa wananchi ili kuendelea kulinda Ikolojia ya Serengeti ambayo sasa ipo hatarini.Pia aliagiza TANAPA kuweka mipaka katika eneo hilo la hifadhi ili kuzuia mifugo inayoharibu mazingira.

**Mheshimiwa Spika**, suala la Mgogoro wa Loliondo ni suala la muda mrefu lililogubikwa na tuhuma mbalimbali za rushwa, usiri, utapeli, na ukitazama kwa undani jambo hili utagundua ujasusi mkubwa wa kiuchumi unaofanywa na mataifa mengine dhidi ya taifa letu kupitia hifadhi zetu na hazina ya wanyama pori katika nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika**, Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka majibu dhidi ya tuhuma zinazowakabili wawekezaji wa kigeni katika Bonde tengefu la Loliondo wanaojishughulisha na shughuli za uwindaji na utalii ambapo serikali zilizopita zimekuwa zikitofautiana kimtazamo juu la suala hili kama ifuatavyo;

- Jeshi la Wananchi wa Tanzania kutoa ulinzi katika kampuni binafsi ya uwindaji na utalii tofauti na ilivyo kwa makampuni mengine ya uwindaji na utalii nchini.
- Uwepo na majengo ya kudumu katika eneo la mapito ya wanyamapori kwenye bonde tengefu la Loliondo kinyume na sheria za uhifadhi.
- Uwepo wa Ikulu ya mfalme katika mapito hayo ya wanyamapori.
- Uwindaji wa wanyama usiozingatia haki za wanyamapori
- Ukiukwaji wa sheria za uhifadhi wa wanyamapori.
- Ukiukwaji wa Sheria ya ugawaji wa vitalu vya uwindaj ndani ya Bonde hilo.
- Ukiukwaji wa sheria za mawasiliano ambapo kampuni ya OBC inayojinasibu kuwa mshirika wa Zantel bado inatoa huduma ya mawasiliano ya simu ya Etisalat ya United Arab Emirates kinyume na sheria za mawasiliano.
- Uwepo wa uwanja mkubwa wa ndege katika eneo la mapitio ya wanyamapori
- Ukiukwaji wa sheria za vijiji na ardhi za vijiji.
- Ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu ikiwemo mauaji, uchomaji wa maboma , vitisho kwa wanahabari wa mgogoro huu kutoka ndani na nje ya nchi
- Tumeshuhudia matamko mbalimbali kutoka ndani na nje ya nchi na hata yale ya watu binafsi.

- Tuhuma za rushwa kwa viongozi mbalimbali katika sekta ya utalii hasa wanaoshughulikia mgogoro huu.
- Tumeshuhudi matumizi ya fedha nyingi na rasilimali za nchi ambapo tume mbalimbali zinazogharimu mamilioni zimeundwa bila manufaa yoyote.

**Mheshimiwa Spika**, Ili kuwa na suluhisho la kudumu kuhusu mgogoro wa Loliondo Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka serikali kufanya yafuatayo;

- o **Kwanza,** serikali kuja na kauli moja kuhusiana na mgogoro wa Loliondo badala ya matamko ya kisiasa yanayokinza na kauli za kubezana kwa watendaji wa serikali kama zile alizozitoa Mkuu wa Mkoa wa Arusha katika mkutano wa wanahabari wakati akitoa taarifa za utendaji wa serikali kwa robo mwaka. Mfano; kwa mujibu wa gazeti la mwananchi la tarehe 02, Februari lililobeba kichwa cha habari ***RC Gambo ampinga Waziri Magembe mgogoro wa Loliondo***, ni ushahidi tosha kuwa serikali haina malengo ya pamoja katika kutatua mgogoro kwani Mkuu wa Mkoa alisema tamko lililotolewa kuhusu kumaliza mgogoro huu ni “***maoni tu***”.Tukumbuke kuwa tamko la Waziri ni suala linalohitaji utekelezaji na sio maoni kama alivyosema Mkuu huyu wa Mkoa.
- o **Pili**, kwa kuwa Waziri aliahidi katika tamko lake kurudisha kwa wananchi eneo lenye ukubwa wa kilometa za mraba 2,500 kwa ajili ya wananchi na mifugo yao , Hivyo basi Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri kuwa; ni vyema sasa eneo hilo likachimbwa mabwawa makubwa ya maji kwa

ajili ya kusaidia mifugo na kupata maji ya uhakika na pia kuepusha wanavijiji kurundikana karibu na maeneo ya mto na pia kulinda ikolojia ya eneo hilo lenye wanyama pori.

- **Tatu**, Serikali kutenga eneo lenye malisho litasaidia pia kuondoa tabia ya wanavijiji kwenda kwenye eneo la hifadhi ili pia kulinda mifugo dhidi ya magonjwa yatokanayo na wanyamapori kwani madhara yake ni makubwa kwa mifugo hiyo na pia ni hatari kwa afya za binadamu.

- **Nne,** serikali itoe majibu kwa tuhuma zinazoikabili kampuni ya OBC pamoja na serikali kama ilivyoelezwa kwenye historia ya mgogoro huu.

- **Tano,** serikali ifanye uchunguzi wa mifugo katika viijiji hivyo kwani kuna malalamiko kuwa nchi jirani pia inaingiza mifugo yake katika eneo hilo la Loliondo. Katika hili Waziri anazo taarifa za kutosha juu ya malalamiko ya wananchi kwa sababu alikumbana na malamiko hayo katika ziara yake fupi aliyoifanya tarehe 25 Januari, 2017 Loliondo.

## 2.3 UANZISHWAJI NA USIMAMIZI WA WILDLIFE MANAGEMENT AREAS (WMAs)

**Mheshimiwa Spika,** kumekuwepo na tatizo kubwa la ujangili ambao umeathiri kwa kiasi kikubwa uwepo wa wanyamapori wa aina mbalimbali katika nchi yetu jambo ambalo pia kwa kiasi kikubwa umeathiri sekta ya utalii kwa ujumla. Ni wazi kuwa mtandao huu wa ujangili umefanywa na watu wenye uwezo mkubwa kiuchumi na pengine kwa kushirikiana na watu wenye madaraka kisiasa au katika

vyombo vya dola. Katika kupambana na tatizo la Ujangili kulianzishwa kitu kinachoitwa Wildlife Management Areas (WMAs).

**Mheshimiwa Spika,** malengo makuu ya kuanzishwa kwa WMA ilikuwa ni ;

- Kushirikisha wigo mpana wa wananchi katika uhifadhi wa wanyamapori (kukasimisha majukumu ya uhifadhi wa wanyamapori kwa wananchi)
- Kuimarisha ulinzi wa wanyamapori nje ya maeneo rasmi ya uhifadhi (yaani hifadhi za taifa,mapori ya akiba n.k)
- Wanavijiji kunufaika moja kwa moja na manufaa yatokanayo na matumizi endelevu ya wanyamapori

**Mheshimiwa Spika**, tangu mwanzoni mwa miaka ya 1990, vijiji vingi vimejihusisha na utalii kwa kutoa maeneo kwa makampuni binafsi katika ardhi zao ili waweze kupata sehemu ya mapato yanayotokana na uwekezaji kwa ajili ya kusaidia shughuli za kijamii. Makubaliano hayo yalisimamiwa na mikataba ya kisheria ikihakikisha vijiji na halmashauri za wilaya wanapata mapato kutokana na utalii wa wanyamapori. Makubaliano hayo yalifanyika kisheria chini ya Sheria ya Serikali za Mitaa (1982) na Sheria ya Ardhi ya Vijiji (1999).

**Mheshimiwa Spika,** WMAs ni motisha kwa jamii ili kuendeleza wanyamapori na kulinda mazingira katika maeneo ya uhifadhi nchini. Motisha hii inaweza kuwa na tija pale tu wananchi wanapopata elimu ya uelewa kuhusu thamani ya wanyamapori katika kukuza uchumi na kuchangia maendeleo katika sekta mbalimbali za kijamii ili kuepusha au kumaliza matatizo ya ujangili katika maeneo yanayozunguka hifadhi yanayofanywa au kuweza kufanywa na baadhi ya watu wasio

waaminifu na hata wageni wanaohujumu nchi yetu kwa kufanya matukio haya ya ujangili.

**Mheshimiwa Spika,** kushirikisha jamii katika mpango huu ni njia mbadala inayoruhusu ubunifu katika mipango ya kulinda na kudumisha shughuli za uhifadhi. Mfano, hivi karibuni vijiji katika Wilaya ya Simanjro wamekubali kutenga ardhi ya vijiji kwa hiari yao ili sasa shughuli za utalii ambazo ni sehemu ya Ikolojia ya Tarangire ziweze kuboreshwa ikiwa ni pamoja na kujenga hoteli za kitalii na kusitisha shughuli za ufugaji na kilimo katika maeneo hayo ili pia kulinda mazalia ya nyumbu.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na uanzishwaji wa kisheria wa WMAs bado kanuni za uendeshwaji na mgawanyo wa mapato baina ya vijiji husika na Serikali kuu hazifuatwi ipasavyo. Jambo hili limekuwa likiibua migogoro ya mara kwa mara baina ya wanavijiji na TANAPA.
Mheshimiwa Spika, WMA zimekuwa na changamoto kubwa hasa katika mfumo wa utozaji kodi na magawanyo wa mapato.Hii ni kutokana na serikali kuchukua kiasi kikubwa cha fedha kinachotokana na mapato ya utaliii kwenye WMA na hivyo kushindwa kutekeleza shughuli za ulinzi wa wanyamapori,kushindwa kufanya shughuli za kuwaletea wanavijiji maendeleo n.k

**Mheshimiwa Spika,** serikali inachukua 55% ya mapato yatokanayo na uwindaji na kuiachia WMA 45%. Vijiji vingi vinategemea mapato ya uwindaji kuliko utalii wa picha. Pamoja na hilo,serikali imekuwa ikikusanya mapato yote ya utalii (yaani mapato ghafi) ambapo mapato hayo hupelekwa kwenye mamlaka ya TAWA yenye akaunti

BOT na fedha hizo huombwa tena kupelekwa kwenye WMA husika.Hii imechelewesha fedha kufika kwenye WMA hizi na fedha hizo hazifiki kwa ufasaha. Mfano;Kambi Rasmi ya Upinzani ya imepata taarifa kuwa WMA ya Burunge-Babati hukusanya takribani shilingi bilioni 6 lakini iliyorudi kwenye WMA ni milioni 800 tu kiasi kwamba maendeleo ya WMA hii yanakuwa ya kusuasua kwa kuwa wananchi hawanufaiki kama inavyopaswa.

**Mheshimiwa Spika,** kumekuwa na changamoto kubwa inayotokana na single entry. Hii ni sera ya TANAPA (TANAPA'' single entry policy) ambayo ni kinyume na malengo ya sera ya Wanyamapori ya mwaka 1998. Single entry policy imesababisha wageni kupungua kwenye WMA ya Ikona na nyingine nyingi. Wageni wengi hukwepa kulipa tozo hizi kwa sababu hazina tija.Utaratibu huu umedidimiza maendeleo ya WMA.

**Mheshimiwa Spika**, mpaka sasa serikali haijatia saini kanuni za uendeshaji wa WMA zilizofanyiwa mapitio mwaka 2012. Mpaka sasa serikali haijatoa sababu zozote ni kwa nini kanuni hizo hazijatiwa saini mpaka leo Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri yafuatayo:

1. Kupunguza masharti ya uanzishaji WMA kwa jamii

2. Kuwe na ufafanuzi na utaratibu wa ugawanaji mafao katika WMA, ili kuhakikisha kuwa asilimia 70% ya mapato kutoka WMA inabaki ngazi ya vijiji kama ilivyoanishwa kwenye kanuni.

3. Kuhakikisha kuwa serikali za vijiji zinapewa  maamuzi ya kisheria kulingana na uwekezaji katika WMA, ikiwa ni pamoja na kuamua

ni kampuni zipi zifanye shughuli za kitalii katika maeneo yao na serikali ibaki na usimamizi wa jumla na maelekezo ya kisera tu.

4. Maeneo ya WMA yaoanishwe na maeneo ya ardhi ya misitu ya vijiji ili jamii wapate manufaa ya juu kutokana na maliasili katika ardhi za vijiji.

5. WMA zilipwe fedha zake moja kwa moja kutoka kwa wawekezaji ili WMA hizi ziweze kulipa mgao wa mapato kwa Serikali Kuu na Halmashauri za Wilaya.

6. Kusimamisha utaratibu wa single entry na tathimini ya athari zake ifanyike

7. Serikali iharakishe kutia (Under certificate of urgency) saini kanuni zilizofanyiwa mapitio kama sehemu ya makubaliano kati ya Wizara ya Maliasili na Utalii na wadau wa uhifadhi yaliyofanyika tarehe 2-3 Julai mwaka 2015.

8. WMA ziweze kujengewa uwezo ili kuweza kujiendesha vizuri

9. Mtazamo wa kisera unahitajika na elimu kwa wananchi kuhusiana na malengo ya WMA's.

10. Kumthibitisha Mkurugenzi wa WMA's ambae amekaimishwa nafasi hiyo kwa takribani miaka miwili sasa ili kuongeza ufanisi katika utendaji.

## 2.4 MIGOGORO BAINA YA VIJIJI NA HIFADHI ZA WANYAMAPORI

**Mheshimiwa Spika**, kumekuwa na migogoro mingi na ya muda mrefu baina ya vijiji na mamlaka za hifadhi. Migogoro hii imekwenda mbali zaidi na katika maeneo mengine kusababisha vifo na familia nyingi kuathirika vibaya kutokana na operesheni za kamata kamata kwa wananchi katika maeneo ambayo yanapakana na hifadhi.

**Mheshimiwa Spika,** Katika Mkoa wa Mbeya, Wilaya ya Mbarali ambapo kumekuwa na mgogoro uliodumu kwa takribani miaka nane baada ya serikali kuamua kuongeza eneo la hifadhi kwa kuingia kwenye vijiji 21 ambavyo hutumiwa na wananchi kwa ajili kujipatia chakula na shughuli zingine za kiuchumi.

**Mheshimiwa Spika,** mwaka 2006 serikali ilitoa maagizo kuwa wataalamu wa maliasili na wataalamu wa ardhi wapitie mapendekezo ya wananchi ambayo kimsingi yalikuwa yanaelekeza ni wapi hasa serikali iweke mipaka kwa makubaliano na wananchi. Hata baada ya hatua hiyo, hivi karibuni limetokea jambo la ajabu ambapo serikali imeanza kuweka kwa siri mipaka ya hifadhi bila kuwashirikisha wananchi.

**Mheshimiwa Spika,** wananchi wa maeneo hayo wameishi katika eneo hilo kwa miaka mingi kabla ya ukoloni kuwepo katika nchini yetu. Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini kuwa wananchi hawa sio wavamizi kama inavyoweza kuelezwa na serikali.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inazo taarifa kuwa kwa sasa wananchi wa vijiji hivi wamekataliwa kuendeleza miundombinu katika eneo hilo. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni

inatambua kuwa wananchi hawa ni wazalishaji wazuri wa chakula, lakini pamoja na hilo hivi karibuni maombi yao ya kutumia *pamp* kwa ajili ya shughuli za kilimo yamesitishwa jambo ambalo limesababisha hasara kubwa sana kwa wakulima kutokana na fedha nyingi walizozitumia katika ujenzi wa miundombinu ya mashamba yao kwa muda mrefu.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatambua kuwa wakati wa kampeni wa uchaguzi mkuu uliopita Rais alipokwenda Mbarali alitoa ahadi kwa wananchi ya kujenga barabara ya Mbarali kwa ajili ya kurahisisha usafirishaji wa mazao yao kwenda viwandani.

**Mhehimiwa Spika**, pamoja na wananchi wa maeneo hayo kupongezwa kwa kilimo kizuri tena kilichozingatia utunzaji wa mazingira leo hii wanaondolewa katika maeneo yao kwa sababu ya upanuzi wa hifadhi wakati ambapo miaka iliyopita walishawahi tena kusogezwa kwa sababu ya upanuzi wa hifadhi hiyo hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka serikali kuja na majibu kuhusiana na mgogoro huu wa wananchi na hifadhi ambapo wananchi wamekuwa wakiishi katika maeneo yao kwa muda mrefu. Aidha Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda kutoa sababu za kwa nini Wizara inapingana na ahadi ya Rais ya kuwasaidia wananchi wa Mbarali ambao hutegemea kilimo ili kuwasaidia katika usambazaji wa mazao yao ya chakula nchini ikizingatia kuwa kutokana na shughuli hizo wameweza kutoa ajira zaidi ya 30,000 na wanachangia uwepo wa viwanda vikubwa 42 na magodown makubwa zaidi ya 56.

## 3.0 MALIASILI NA UTALII

## 3.1 ATHARI ZA ONGEZEKO LA KODI KATIKA SEKTA YA UTALII NCHINI

**Mheshimiwa Spika,** suala la mrundikano wa kodi kwa wafanyabiashara katika sekta ya utalii sio suala geni. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikilizungumzia jambo hili mara kwa mara kutokana na jinsi linavyowaumiza wadau wa sekta ya utalii nchini pamoja na wananchi wengine wanaotegemea shughuli za utalii kujipatia riziki.

**Mheshimiwa Spika**, katika hotuba ya Kambi ya Rasmi Upinzani wakati wa mkutano wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ilizungumzia suala la ongezeo la kodi ya VAT na ikionyesha madhara makubwa yanayoweza kujitokeza endapo serikali itapandisha kodi hii kwa ghafla.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na uchambuzi huo uliofanywa na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, serikali iliamuru wafanyabiashara hao kulipa kodi hiyo mara moja na jambo ambalo limewasababishia wafanyabiashara hasara kubwa. Kutokana na kuyumba kwa biashara ya utalii nchini na pia ongezeko kubwa la kodi; wafanyabiashara hao walilazimika kupunguza wafanyakazi na hivyo serikali ilikosa kodi ya mapato inayotokana na mishahara ya wafanyakazi (PAYE). Aidha, baadhi ya wamiliki wa makampuni na hoteli wamelazimika kuuza hoteli na makampuni yao na kusababisha usumbufu kwa wageni kwani wengi walilazimika kuchangia ongezeko hilo la kodi.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na hilo kuna takribani zaidi kodi 36 ambazo wafanyabiashara wa utalii nchini wanalazimika kulipa wafanyabiashara wa utalii nchini. Kodi hizo ni kama ifuatavyo;

1. TALA License
2. EWURA tax 1% charged by TANESCO from October 2009
3. REA tax 3% charged by TANESCO from October 2009
4. VAT
5. Corporation Tax
6. Withholding Tax
7. Stamp duty
8. Occupational and Safety Health Authority compliance certificate (OSHA)
9. Park fees to tourists
10. Crew Park entry fee-Mountain climbing
11. Guides licence
12. Annual vehicle road license fees
13. Safety week stickers
14. Land rent
15. Property tax
16. N.S.SF
17. Skills and Development Levy
18. Municipal Service Levy (Kodi ya huduma 0.3% ya pato)
19. Bedding levy hotels
20. Concession Levy-hotels
21. Registration of vehicles
22. Import duty
23. Local Community fees

24. Bar license- hotel

25. Camping fees to TANAPA

26. Ngorongoro Crater service fees

27. Rescue fees –Mountain climbing

28. Excise duty of 0.15% charged by banks on payments

29. Tourism development levy introduced from October 2013

30. Business License fees paid to Ministry of Industry and trade

31. Residence permit fees

32. Radio license fees paid to TCC

33. Wildlife management fees

34. SUMATRA fees paid to surface and Marine Transport Regulatory Authority

35. Workman's ccompensation fund

36. Forest fees

**Mheshimiwa Spika**, hizi ni baadhi tu ya kodi katika sekta ya utalii nchini Tanzania. Mrundikano huu wa kodi hasa kwa wafanyabishara wazawa ni taswira tosha kwa wananchi wetu kujua namna serikali ya awamu ya tano ya Chama cha Mapinduzi inavyowakamua.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa gazeti la mwananchi la tarehe 04 Februari, 2016 katika makala ya uchumi yenye kichwa cha habari kuwa **"Wingi wa kodi unavyoua utalii Tanzania"** limeleeza kwa kina utafiti uliofanywa na Dr. Hawa Eve Sinare unaoonyesha ili mfanyabiashara wa utalii Tanzania aweze kulipa kodi, kutimiza masharti ya leseni na malipo mengine inamlazimu kutumia takibani masaa 2,000 kwa mwaka. Hii ni kutokana na wingi wa masharti kwa

wafanyabiashara wa ndani na nje katika sekta ya utalii ikilinganishwa na sekta nyingine.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa sasa Tanzania ina takribani kampuni 1,050 zinazofanya biashara ya utalii lakini ni kampuni 300 tu ndio zilizoweza kutimiza masharti ya kulipa kodi kutokana na wingi wa kodi na mfumo mzima wa ulipaji kodi. Ni jambo la ajabu kabisa  kwani ni rahisi zaidi kulipa faini kwa kosa la kufanya biashara kinyume na sheria kuliko kutekeleza masharti ya ulipaji kodi.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kuziangalia upya kodi zinazowaumiza wafanyabiashara ya utalii nchini, lakini pia serikali haina budi kuanzisha '*one stop centre'* kwa ajili ya malipo ya kodi katika sekta ya utalii kwani kumekuwa na usumbufu katika ulipaji. Vilevile serikali iondoe mkanganyiko katika udhibiti na usajili unaojirudia rudia bila sababu kutoka kampuni za usajili nchini. Hii ni kwa sababu kati ya kodi 36 zinazolipwa kodi 12 ni za usajili na leseni pekee.

### 3.2 KUANZISHA BUSTANI YA WANYAMA KATIKA MSITU WA PANDE

**Mheshimiwa Spika**, Pori la akiba lijulikanalo kama Msitu wa Pande limekuwa ni msitu wenye historia ya kipekee na ya kutisha sana. Msitu huu uliopo takribani kilometa 25 kutokea Jiji Dar es Salaam kuelekea Bagamoyo ni msitu wenye wanyama wadogo wadogo na mimea ya kipekee ambayo haipatikani katika maeneo mengine yoyote.

**[MANENO YAMEONDOLEWA KWA MAELEKEZO YA SPIKA]**

**Mheshimiwa Spika,** mwaka 2015 ndani ya Bunge hili Mheshimiwa John Mnyika aliwahi kuuliza swali la nyongeza kuhusiana na ahadi ya serikali katika kuuendeleza msitu ili uwe sehemu ya utalii kama sehemu ya matumizi bora ya misitu ambapo ahadi hii ya kuufanya msitu huu kuwa sehemu ya utalii ni ahadi ya serikali ya muda mrefu na serikali ilishawahi kutangaza zabuni ambayo mpaka leo haijulikani ni nini kilichoendelea.

**Mheshimiwa Spika**, katika majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri alijibu kama ifuatavyo***: " nimpongeze Mheshimiwa Mnyika kwa mtanzamo chanya wa kwamba anakubaliana na dhana nzima ya matumizi bora ya maeneo ya misitu;hapingani na dhana nzima ya serikali kuhusiana na kuifanya misitu iwe ni rasilimali ambayo inaweza kutumika kwa ajili ya maslahi ya jamii;kuhusu suala la kwamba kuna ucheleweshaji kama ambavyo amesema;nataka nimtoe wasiwasi kwamba historia inatukumbusha tulipotoka,mahali tulipo na inatuwezesha kuona kule ambako tunakwenda.Nataka Mheshimiwa Mnyika akubaliane tu na rai yangu kwamba tumetoka huko tulikotoka,mipango imekuwepo lakini awamu hii mipango hii ninayoizungumzia ni uhakika na kwamba awamu hii nataka anipe muda wa mwaka mmoja tu,halafu aweze kuona katika eneo hili tunafanya nini".***

**Mheshimiwa Spika***,* hayo ndiyo yaliyokuwa majibu ya serikali mwaka 2015, japo jambo hili limezungumziwa muda mrefu hata kabla ya mwaka 2015. Hii inaonyesha kwamba serikali ya Tanzania inazungumza na kutoa ahadi lakini haitekelezi inayoyazungumza. ***(The government of Tanzania talks the talk but it doesn't walk the walk).*** Kutokana na tabia ya serikali kutoa majibu mepesi yasiyo na

utekelezaji, mpaka leo hakuna jitihada zozote zilizofanyika ili kuhakikisha utekelezaji wa ahadi ya serikali.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kutoa mfano wa Nchi ya Kenya ambapo katika jiji la Nairobi kuna Msitu wa Karura (Karura forest) ambao umekuwa ni kivutio kwa wakazi wa Nairobi na wageni wanaotembelea nchi hiyo. Msitu wa Karura umekuwa ukichangia uhamasishaji na utangazaji wa shughuli za utalii nchini Kenya.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali ya CCM kujisahihisha katika hili, kwani nchi haijengwi kwa maneno bali matendo. Ifike mahali sasa majibu na ahadi za serikali ziweze kutekelezwa kwani tabia ya serikali kushindwa kutekeleza ahadi kunazidi kuchelewesha maendeleo ya taifa hili. Ni muhimu sasa serikali ikawa na wivu wa kimaendeleo kwa taifa lake na watu wake. Kambi Rasmi ya Upinzani inatamani kuona kila kiongozi wa serikali akijikita kwa dhati katika kutatua changamoto za kimaendeleo na sio kujikita katika siasa pekee..

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kushauri kuwa ni wakati mwafaka sasa serikali kuanzisha bustani ya wanyama katika Msitu wa Pande na hivyo kuwa sehemu ya utalii kwa wananchi wa Mkoa wa Dar es Salaam pamoja na watalii wengine wanaotembelea nchi yetu. Bustani hii inaweza kuwa sehemu ya wananchi kuwa na maeneo ya kupumzika mwishoni mwaka au wiki na hivyo kuliongezea taifa mapato.

### 3.3 RUAHA NATIONAL PARK

**Mheshimiwa Spika**, hifadhi ya wanyama ya Ruaha ni hifadhi yenye historia kubwa na ilianza kutambulika zaidi mwanzoni mwa mwaka 1877 pale ambapo iliingia rasmi katika machapisho mbalimbali. Hifadhi hii inauwanda mzuri sana wenye wanyama wengi.Ni moja ya hifadhi kubwa zaidi katika ukanda wa Afrika Mashariki

**Mheshimiwa Spika,** bado serikali haijaitangaza hifadhi hii muhimu kwa ukanda wa kusini (Southern circuit). Idadi ya watalii wanaofika katika ukanda huu wa kusini ni wachache na hiyo yote inasabishwa na kukosekana kwa matangazo ya kutosha ili kuvutia watalii wengi kutembelea hifadhi hii.

**Mheshimiwa Spika,** bodi ya utalii nchini (TTB) iko taabani kutokana na wingi wa madeni inayoikabili na pia bajeti yake ni ndogo sana jambo linaloipelekea TANAPA na NCAA kuchangia gharama za maonyesho mbalimbali ndani na nje ya nchi. Iwapo TTB inashindwa kujiendesha tunategemea vivutio hivi vitaweza vipi kutangazwa?

**Mheshimiwa Spika,** maeneo ya kuzunguka hifadhi ya Ruaha hayana hoteli nyingi zenye hadhi za kimataifa. Mpaka sasa kumekuwa na malalamiko makubwa kutoka kwa wafanyabiashara na wadau wa utalii kwani kuna hoteli inayotegemewa katika eneo hilo ambayo hutoza gharama kubwa sana jambo ambalo wageni wengi hushindwa kutembelea eneo hilo.

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na hilo usafiri mkubwa unaotegemewa ni wa ndege ndogo ambapo gharama yake ni kubwa. Kwa kuwa serikali imeshindwa kuendeleza eneo hili la hifadhi ili wageni waweze kutembelea kwa wingi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kutengeneza barabara ili wageni wanaotembelea eneo hilo waweze kutumia usafiri wa barabara. Mheshimiwa Spika, Endapo

barabara hii itatengenezwa basi wageni wanaotembelea hifadhi hii wanaweza kutembelea mpaka mbuga ya Mikumi kwa urahisi zaidi baada ya kuboresha miundombinu ya barabara ya hifadhi hizo mbili.

**Mheshimiwa Spika,** vilevile Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inasisitiza kuwa serikali ipunguze msusuru wa kodi kwa wafanyabiashara katika sekta hii ili sasa makampuni binafsi yaweze kuwekeza katika eneo la hifadhi ya Ruaha na hifadhi nyingine zilizopo Southern circuit ikiwa ni pamoja na kujenga hotel zenye hadhi ikiwa ni pamoja na lodge na camp site.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kuandaa mpango mahususi wa kuwaalika wawekezaji ***kwa vitendo*** kutoka ndani na nje ya nchi ili sasa waweze kuzungumzia namna bora ya kuwekeza katika ukanda huo,lakini pia serikali iweze kuisaidia TTB ili itangaze vivutio hivi zaidi.

### 3.4 SERIKALI KUSHINDWA KUVUMBUA VIVUTIO VIPYA VYA UTALII

**Mheshimiwa Spika,** kwa miaka mingi sasa serikali yetu imekuwa ikitegemea mbuga za wanyama, milima, bahari, uchongaji wa vinyago na kutembelea mali kale kama sehemu kuu za utalii katika nchi yetu. Serikali imejifunga katika vivutio hivyo nilivyoreje japo kuna utalii wa aina nyingine mwingi ambao unaweza kuongeza pato la nchi na kuwaletea wananchi maendeleo binafsi na taifa kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** kati ya nchi zilizofanikiwa sana katika utalii ni pamoja na nchi za Uingereza, Ujerumani, Uturuki, Italia, China, Hispania, Marekani na Ufaransa. Mfano, kwa mujibu wa habari mbalimbali zinazopatikana katika tovuti mbalimbali za utalii zinabainisha kuwa katika nchi ya Ufaransa takribani watalii milioni 83.7

walitembelea nchi hiyo kwa mwaka 2014 pekee. Ufaransa ni nchi inayotegemea sana jengo la mnara wa Eifel (Eifel tower), Kasri la mfalme (Palace of Versailles) n.k Nchi hii inategemea sana maeneo ya kihistoria katika taifa la Ufaransa. Hii ikiwa ni majengo ya kale, sanamu za kumbukumbu, makumbusho na sehemu za mito na fukwe.

**Mheshimiwa Spika,** maeneo haya yanaipatia ufaransa fedha nyingi za kigeni na yanachangia kwa kiasi kikubwa pato la taifa la Ufaransa. Hapa kwetu Tanzania mambo ni yaleyale (business as usual). Tumeshindwa kutengeneza akili mpya za kufanya tafiti kwa kina kwenye vivutio vipya pamoja na kuongeza bajeti ya maendeleo ili tafiti ziweze kufanyika ipasavyo. Kutokana na sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imeona ni wakati muafaka sasa wa kupendekeza mambo mapya na vivutio vipya vya utalii ili kuweza kuisaidia serikali.

**Mheshimiwa Spika,** miaka ya hivi karibuni kumekuwa na kauli mbalimbali za kutaka kujua katikati mwa Tanzania ni wapi ili kuweka alama itakayotumika kama sehemu ya kihistoria na sehemu ya utalii wa nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika**, katika vyanzo mbalimbali vya habari vinaonyesha kuwa katikati mwa Tanzania ni kijiji cha Sukamahela kilichopo kata ya Solya wilayani Manyoni mkoani Singida. Hii ni kutokana na uwepo wa chuma kilichopo kijijini hapo kinachosadikiwa kuwa ndipo eneo rasmi la katikati ya Tanzania.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na taarifa hizo za Kijiji cha Sukamahela, vyanzo vingine vinaonyesha kuwa kitongoji cha Darajani kijiji cha Chisinjisa kata ya Sasilo, tarafa ya Nkonk'o Wilaya ya Manyoni ndipo eneo la katikati mwa Tanzania. Katika makala ya gezeti la

Mwananchi la tarehe 25, Januari 2015 lilieleza kwa kina aina ya vipimo mbalimbali vilivyotumiwa na serikali ya Ujerumani wakati wa ukoloni na vipimo vipya vilivyofanywa na serikali ya Tanzania chini ya mpima ardhi mkoani Singida.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatambua jitihada mbalimbali zilizofanywa na waandishi wa habari na wadau wengine kutaka kujua ni wapi hasa eneo la kitovu cha Tanzania lilipo ili sasa waweze kusaidiana na serikali katika kutengeneza eneo hilo kuwa sehemu nzuri ya kihistoria na utalii badala ya ilivyo sasa kwani maeneo haya hayajatambuliwa rasmi na serikali.

**Mheshimiwa Spika**, Tukumbuke kuwa Mwalimu Nyerere aliwahi kujenga nyumba katika eneo la Sukamahhela ili kuwasaidia Wazee waliokosa makazi na kwa sasa hali ya makazi hayo sio nzuri hivyo wengi hulazimika kukaa kando kando ya barabara kwa ajili ya kuomba riziki kutoka kwa abiria na wasamaria wema wanaopita maeneo hayo.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na hilo mkoani Kilimanjaro katika Wilaya ya Same kuna Mlima ya Shengena ambao ni maarufu kwa ufugaji wa ngo'mbe wa asili ambao huitwa kwa miluzi na wanajichunga wenyewe, kuna uwanda mzuri kwa ajili ya watalii kufanya camping, kuna ziwa Kenyabasa kule Mkoani Kagera ambalo ni ziwa la maajabu kutoka kwenye chungu,tuna kimondo cha Mbozi,maajabu ya mto Kiwira ambapo mto huingia ndani ya shimo dogo la miamba, maji moto (hot springs katika kijiji cha chemka wilaya ya Hai , hotsprings za Mkoani Mbeya, kuna udongo unaohama (shifting sand dunes) mkoani Manyara ambapo eneo hili halijatangazwa ipasavyo, makumbusho ya Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere mkoani Mara,

maporomoko ya maji ya mto Rusumo, muonekano mzuri wa Ziwa Chala, tuna milima ya Kolero yenye historia na maajabu yake na mti wa maajabu ulioishi miaka zaidi ya 500 katika Wilaya ya Moshi Vijijini.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kuwa na wataalamu wa kufanya tafiti kwenye vivutio vipya vya utalii nchini. Kitendo cha serikali kuendelea kukumbatia vituo vilevile ambavyo matokeo yake ni yaleyale ni kitendo cha kuendelea kuididimiza sekta ya utalii nchini. Bajeti inayotengwa na serikali ni lazima iweke kipaumbe katika kufanya tafiti ili kuwepo na vivutio vyenye tija ambavyo vitafikika kwa urahisi na vitaweza kuwavutia watalii wengi.

### 3.5 VAZI LA TAIFA NA MANUFAA YAKE KATIKA SEKTA YA UTALII

**Mheshimiwa Spika,** kwa muda mrefu sasa Tanzania imekuwa na mchakato usiokamilika wa kutafuta vazi la taifa. Jambo hili la muda mrefu limeshindwa kukamilika kutokana na kuwepo kwa siasa na ukinzani usio na tija katika kutafuta vazi litakalotuunganisha kama taifa moja. Tangu Mwezi Desemba, 2011 aliyekuwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo aliunda kamati maalum ya kutafuta vazi la taifa ambalo kamati nyingi zimeundwa baada ya hapo.

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na kuzuka kwa maswali mengi katika mchakato huu wapo wananchi wengi wanaojiuliza kwamba ikiwa serikali imeshindwa kupata vazi la taifa, huku wadau wa mitindo ya mavazi nchini wakifanya vizuri katika medani za ndani na nje ya nchi,Je, serikali inatuhakikishia vipi kuwa inauwezo wa kutoa kwa utoshelevu bajeti iliyotengwa katika Wizara hii?

**Mheshimiwa Spika,** nchi nyingi duniani zimeweza kujitambulisha vyema kutokana na mavazi yao. Nchi kama Rwanda ina vazi lake la asili lijulikanalo kama Mshanana nchi kama Uganda ina vazi lake lijulikanalo kama Gomesi au Busuuti n.k Hata baadhi ya nchi katika mataifa ya Ulaya, Asia, na kwengineko nao wanamavazi yao yanayotambulisha utaifa wao na yamekuwa sehemu ya kivutio kikubwa kwa watalii.

**Mheshimiwa Spika,** ni rahisi sana kwa taifa kuiga mambo mengi kutoka kwenye mataifa mengine lakini kamwe hakuna taifa linaloweza kuiga utambulisho na utamaduni wa mataifa mengine. ***Kushindwa Kwa taifa kuwa na utambulisho wake Kwa kupitia watu wake, ni utajiri wa umaskini.***

**Mheshimiwa Spika**, Mchakato wa kupata vazi la taifa kama utambulisho na sehemu muhimu ya utamaduni hauwezi kufikia hitimisho kwa kupelekwa kwa wananchi kama ilivyoelezwa na Wizara ya Utamaduni na Michezo katika hitimisho la hoja ya Bajeti ya Wizara hiyo na kuachwa bila usimamizi maalumu na hamasa kwa wananchi.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kuangalia upya mchakato huu, ifanye tathimini ya kina kuona ni kwa namna gani kuwepo kwa vazi la kitaifa kutaleta manufaa kwa nchi hususani katika sekta ya utalii nchini. Katika kulingalia hili serikali iwe na mpango wa hamasa na elimu kwa wananchi kuona umuhimu wa kuwa na vazi hilo kuliko ilivyo sasa ambapo serikali imejitoa katika suala hilo na kuwaachia wananchi wenyewe wakati imetumia fedha nyingi kuunda kamati kwa ajili ya suala hilo.

### 3.6 USHIRIKISHWAJI WA DIASPORA KATIKA KUTANGAZA UTALII

**Mheshimiwa Spika,** biashara yoyote inahitaji matangazo ili iweze kufanya vizuri zaidi. Katika kufanya matangazo hayo mbinu mbalimbali zinaweza kutumika. Kwa hapa nchini Bodi ya Utangazaji wa vivutio vya utalii nchini imekuwa ikikumbwa na changamoto mbalimbali zikiwemo changamoto za kifedha katika kufanya maonyesho mbalimbali, kutoa machapisho na matangazo kwa njia ya kieletroniki.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi rasmi ya Upinzani inapendekeza kuwa ni wakati sasa wa kuwa na kitengo cha utalii cha Diaspora ambacho kitafanya kazi ya kutangaza vivutio vyetu ikiwemo vivutio vipya ambavyo vitatambuliwa. Pamoja na hilo Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa ni wakati sasa wa kuhamashisha Diaspora investment kwenye sekta ya utalii. Hii ni pamoja na kuhamasisha sekta binafsi kuweza kuwekeza zaidi kwenye sekta ya utalii.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na hili Diaspora tourism na uhamasishwaji wa sekta binafsi hautaweza kuwa na mafanikio endapo serikali haitachukua hatua za makusudi katika kupunguza kero zilizopo kwa wafanyabiashara katika sekta utalii ikiwemo wingi na ugumu wa masharti katika kuanzisha na kuendesha biashara ya utalii nchini pamoja na orodha ndefu ya kodi katika sekta hii.

## 4.0 WANYAMA PORI

### 4.1 TATHIMINI YA UDHIBITI WA BIASHARA YA PEMBE ZA NDOVU

**Mheshimiwa Spika,** serikali, mashirika ya umma, sekta binafsi na taasisi mbalimbali za kitaifa na kimataifa zimekuwa zikipinga sana ujangili dhidi ya Ndovu unayofanywa na watu wasiolitakia mema taifa letu.

Pamoja na jitihada mbalimbali zinazoendelea kufanyika bado mpaka sasa ujangili dhidi ya Ndovu unaendelea.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Sensa iliyofanywa na Taasisi ya utafiti wa wanyamapori Tanzania (TAWIRI) kuwa Mwaka 1979 idadi ya Ndovu ilikuwa takribani Ndovu 316,300, mwaka 2006 idadi ya Ndovu ilikuwa 136,753, mwaka 2009 idadi izidi sana kupungua mpaka Ndovu 109,051 na mwaka 2015 imepungua zaidi ya asilimia 60 na kufikia idadi ya Ndovu 50,443.

**Mheshimiwa Spika**, jambo hili ni la kusikitisha sana. Serikali imeshindwa kulinda rasilimali za nchi hii kwa wivu wa hali ya juu kiasi kwamba tangu mwaka 1979 serikali imeshindwa kabisa kuzuia biashara hii haramu japo kuna matamko mengi jambo ambalo linazua maswali mengi kuwa ni akina nani hasa wanufaika wa biashara hii haramu?.

**Mheshimiwa Spika**, Hata hivyo, mwaka 2014, Tanzania ilitia saini mpango wa kuwalinda Ndovu (Elephant Protection Initiative).Mpango huu ulizuia uuzaji wa pembe za Ndovu kwa muda wa miaka kumi. Pamoja na hilo Tanzania kuna ghala ya meno ya Ndovu/Tembo yenye uzito wa tani laki moja na kumi na nane kwa mujibu wa BBC News 2014.

**Mheshimiwa Spika,** ghala hili linagharimu takribani dola 75,000 kwa mwaka sawa na shilingi 167,925,439.19 kwa exchange rate ya shilingi 2,239.01 ya tarehe 20, May 2017 lakini pamoja na hilo pendekezo la Tanzania kwa CITES mwaka 2009, serikali ilisema kuwa ghala la kuhifadhi meno hayo ya tembo limejaa na hivyo serikali itahitaji dola milioni moja kujenga lingine ambayo ni sawa na kiasi cha shilingi 2,239,005,855.82

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka serikali kufanya yafuatayo:

- Kuzuia kabisa biashara ya meno ya tembo na sio kusitisha kwa kipindi cha miaka kumi pekee. Serikali itambue kusitisha biashara hiyo pengine ni kuwapumzisha tu majangili.Inachukuwa takribani miezi 22 kwa tembo mmoja kuzaa lakini ni kitendo cha dakika tu kumuua tembo mmoja.

- Mpaka sasa ghala linalotumika kuhifadhi meno ya tembo halina utaratibu mzuri wa kuhifadhi pembe zilizokamatwa. Na hivyo ni rahisi biashara hii kuendelea kufanyika kwa kutumia pembe zilizo ndani ya ghala hilo kwa nia haramu. Hii ni kutokana na uhifadhi wa hovyo unaofanyika ndani ya ghala hilo.Pembe hizi hazina alama maalumu na za kisasa ili kuweza kuzifuatilia kitakwimu na kwa makundi yao ya sifa za kisayansi.

- Mpaka sasa ghala hili linagharimu fedha nyingi sana huku wananchi wakiwa hawana huduma muhimu kama chakula, maji, nishati n.k. Fedha hizi pia zingeweza kabisa kutumika katika kuweka mazingira ya kudhibiti ujangili nchini. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inahoji ni kwa nini sasa serikali isiweze kuziteketeza pembe hizi kama walivyofanya Kenya, China n.k kwani kuyapeleka sokoni ni kutoa motisha kwa majangili kuendelea kujipenyeza katika biashara hii.

- Serikali ituambie mpaka mwaka huu wa 2017 kuna tani ngapi za pembe za Ndovu zilizo katika ghala hilo kwani takwimu nyingi zinaonyesha kiwango cha pembe hizi mpaka mwaka 2014 pekee.

## 4.2 SEKTA YA WANYAMAPORI NA BIASHARA YA UWINDAJI NCHINI

**Mheshimiwa Spika,** Wanyamapori ni rasilimali endelevu kwa Tanzania ukilinganisha na rasilimali zingine kama madini na mafuta. Jambo la muhimu katika sekta hii ni kuwa na sera pamoja na matendo yenye usimamizi endelevu wa wanyamapori na hivyo shughuli za kiuchumi zinazotokana na wanyamapori zitaendelea kukua na kupanuka kwa miongo mingi ijayo.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na bahati hiyo ya kuwa na wanyama wengi, Tanzania ina Mtandao mkubwa wa maeneo yaliyohifadhiwa yaani (Protected Areas) ambayo huchukua takribani asilimia 28 ya ardhi yote ya Tanzania. Kati ya asilimia hiyo, asilimia 4 ni hifadhi za Taifa (National parks), asilimia 1 ni Hifadhi ya Ngorongoro (NCA), asilimia 15 ni Mapori ya Akiba (GRs) na asilimia 8 ni Mapori Tengefu (GCAs). Aidha, hifadhi za misitu takribani 150 huchukua asilimia 15 ya ardhi yote ya Tanzania.

**Mheshimiwa Spika,** dhana halisi ya uwindaji wa kitalii ina maana ya matumizi endelevu ya wanyamapori ambayo yana faida kiuchumi. Hii inajumuisha uchumi endelevu unaoendana na sera ya utalii kuhusu uwindaji kwa kiwango kidogo lakini chenye tija na kinachoweza kuchangia kwa kiwango kikubwa katika uchumi wa taifa.

**Mheshimiwa Spika**, kwa hali halisi ilivyo sasa maeneo mengi ambayo uwindaji umekuwa ukifanyika kumekuwepo na kuripotiwa madhara makubwa kuliko faida. Hii ni kutokana na wanyama wengi kuuawa bila kuzingatia sheria, kuuawa kwa wanyama wadogo, kupotezwa kwa baadhi ya viumbe kwa njia za kibaiolojia bila hata serikali

kutambua na hii imetokea katika mataifa mengi duniani kwa sababu za kiuchumi na kisiasa (economic and political conspiracy).

**Mheshimiwa Spika,** ukiukwaji huu mkubwa wa sheria za uwindaji umefanyika sana hapa nchini na katika kumbukumbu Kambi Rasmi ya Upinzani iliwahi kuzizungumzia sana Kampuni za Uwindaji za Green Miles na OBC zilizokumbwa na baadhi ya shutuma hizi.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inazo taarifa kuwa mpaka sasa wanyama kama DUMA (Cheetah), Faru, Tembo, Mbwa mwitu n.k wanaendelea kutoweka katika hifadhi zetu jambo linaloilazimu serikali kuagiza wanyama kutoka nje ya nchi kama vile Faru ili kusaidia uzalishaji wa wanyama hawa jambo ambalo linaigharimu serikali fedha nyingi kutokana na uzembe tu wa serikali kushindwa kulinda rasilimali zake, kuwakumbatia watendaji waovu na wabinafsi wanaotazama maslahi yao binafsi kuliko maslahi ya taifa.

**Mheshimiwa Spika**, baadhi ya mifano ni gharama kubwa iliyotumika kumnunua Faru John na shilingi milioni 64 ambazo hutumika kila mwezi kumtunza Faru Fausta ambae haingizi pato lolote kwa sasa na jambo hili ni matumizi mabay ya fedha za umma na kukosa vipaumbele kama taifa .Tukumbuke fedha hizi zinatumika wakati mamilioni ya wananchi wa Tanzania hawana huduma za afya, uhakika wa upatikanaji wa chakula, kukosa shule zenye ubora na wanakabiliwa na shida kubwa ya maji, nishati ya umeme, bei ghali za bidhaa ikiwemo sukari na unga pamoja na matatizo mengine lukuki.

**Mheshimiwa Spika**, kumekuwa na tuhuma za rushwa kwa wanaojishughulisha na biashara hii ili kupata vitalu vya uwindaji kwa muda mrefu. Katika mtandao wa Jamhuri ya tarehe 23 Mwezi August, 2012 ilizungumzia jambo hili kwa kina sana.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatambua kuwa katika utekelezaji wa Sheria Namba 5 ya mwaka 2009 inaelekeza kwamba kampuni za kigeni zisizidi asilimia 15 ya kampuni zote zinazogawiwa vitalu. Lakini mpaka sasa takribani asilimia kubwa ya kampuni zilizogawiwa vitalu zinamilikiwa na wageni.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatambua kuwa biashara ya uwindaji inayohusisha kusafirisha wanyama pori wakiwa hai ilipigwa marufuku rasmi kufuatia tamko la Waziri Mkuu Bungeni tarehe 18,Agosti 2011. Lakini pamoja na hilo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kufanya yafuatayo;

1. Kuitaka TAKUKURU ichunguze kwa kina kama kuna kampuni yoyote bado inasafirisha wanyama hai kwa siri wakiwemo wanyama wakubwa na wale watambaao kama vile mijusi,kenge, nyoka, tumbili , vipepeo n.k kwani hata hao walishakatazwa kufuatia tamko la Waziri wa maliasili na utalii mwaka jana.
2. Serikali ilete muswada Bungeni kuhusu sheria ya uwindaji ili Bunge lipate fursa ya kupitia na kuangalia upya namna nchi itakavyoweza kunufaika na biashara ya uwindaji, na vilevile kuangalia namna ya kuwalinda wanyama na viumbe vingine ndani ya hifadhi ili kuhakikisha hatupotezi kiumbe hai cha aina yoyote ‘species’.

3. Serikali ifanye upembuzi yakinifu (thorough analysis) kuhusiana na faida na hasara za uwindaji, kiasi cha uwindaji kinachofanyika nchini ikilinganisha na idadi ya wanyama waliopo, ifanye tafiki kuhusiana na uwepo wa viumbe vipya au kupotea kwa baadhi ya viumbe katika mbuga zetu ili sasa taifa liweze kuamua kusitisha au kuendelea na biashara ya uwindaji wa wanyamapori na viumbe hai.

## 4.3 UGAWAJI WA MAENEO YA HIFADHI BILA KUZINGATIA TARATIBU ZA KULINDA WANYAMAPORI NA MISITU

**Mheshimiwa Spika**, hivi karibuni Mamlaka ya hifadhi ya Ngorongoro imetuhumiwa kugawa eneo la msitu wa asili katika kijiji cha Olchniomelole kwa kampuni ya utalii inayojulikana kama Asilia. Kampuni hii inamiliki hoteli za aina mbalimbali kama lodges na campsite. Kwa mujibu wa taarifa mbalimbali kutoka kwa wananchi wa eneo hilo wamelalamikia tabia ya Mamlaka ya NCAA kugawa kiholela maeneo ya hifadhi na huku kukiwa na tuhuma za rushwa dhidi ya mamlaka hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** kuna lodge na campsite zaidi ya 30 zilizojengwa kandokando ya kingo za kreta ya Ngorongoro jambo ambalo linaweza kuathiri uhai wa kreta, ikolojia ya eneo la kreta pamoja na viumbe hai wanaopatikana ndani ya kreta.

**Mheshimiwa Spika**, Uharibifu huu unaofanywa ndani ya kreta unaharibu pia barabara za kuingia na kutoka ndani ya kreta kwa kuwa magari makubwa ya vifaa vya ujenzi yanaingia ndani ya kreta

mbapo kimsingi barabara hizi hazina uwezo wa kubeba magari makubwa yenye mizigo mara kwa mara. Jambo hili sio tu limelalamikiwa na wananchi bali pia jumuiya za kimataifa zinazoshughulikia mazingira ya uhifadhi.

**Mheshimiwa Spika,** zipo tuhuma za majina ya maafisa mbalimbali wanaotajwa kushiriki vitendo vya rushwa na kukosa maadili ya kazi.Ni dhahiri vitendo hivi visipo dhibitiwa vinaliingiza taifa katika hasara kubwa ikiwemo kuharibika kabisa kwa Ikolojia ya Ngorongoro ambayo ndio eneo pekee duniani ambapo binadamu wanaishi eneo moja na wanyamapori.

**Mheshimiwa Spika**, Kitendo cha kuharibu Ikolojia hii kwa ujenzi wa majengo makubwa ya kudumu ni kitendo kinachopeleka kupungua kwa malisho na maji kwa wanyama na mifugo iliyopo ndani ya hifadhi hii kwani mpaka sasa idadi ya watu na mifugo ndani ya kreta inaongezeka sana.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaishauri serikali kufanya yafuatayo:

1. Serikali kuchukua hatua za dharura ili kufanya uchunguzi wa tuhuma hizi, na pia kufanya tathimini ya ugawaji wa ardhi katika eneo la kreta.

2. Serikali ichunguze tuhuma za eneo la ardhi ya msitu lililotolewa kinyemela kwa kampuni ya Asilia, pamoja na makampuni mengine yaliyojenga hoteli mbalimbali kwenye kingo za kreta. Vilevile, serikali iangalie kama maeneo hayo yalitolewa kisheria na kwa ukubwa ule ule uliopaswa kutolewa kwa kampuni hizo.

Endapo maeneo hayo yalitolewa kisheria na yalifuata taratibu serikali ituambie je, kuruhusu ongezeko la ujenzi wa majengo ya kudumu kando kando ya kreta lina athari gani kwa Ikolojia ya kreta siku za usoni?

3. Serikali ichunguze tuhuma hizi za rushwa na utovu wa nidhamu ya maadili ya kazi zinazowakabili watendaji ndani ya Mamlaka ya hifadhi ya Ngorongoro.

## 5.0 MISITU NA NYUKI

### 5.1 ZUIO LA MATUMIZI YA MKAA NA KILIO KWA WANANCHI

**Mheshimiwa Spika,** moja ya majukumu ya Wakala wa Misitu nchini (TFS)ni kusimamia rasilimali za misitu ili ziweze kusaidia ustawi wa taifa kwa sasa na vizazi vijavyo. Hivyo hatuna budi kama taifa kulinda rasilimali za misitu kwa nguvu zote. Kambi Rasmi ya Upinzani inaunga juhudi za kutunza misitu ikiwa ni pamoja na kuwajengea wananchi utamaduni wa kupenda kupanda miti maeneo yanayozunguka mazingira yetu.

**Mheshimiwa Spika,** serikali imekuwa ikitoa matamko ya kukataza matumizi ya mkaa kwa miaka mingi. Japokuwa matakazo haya ya matumizi ya mkaa ni ya muda mrefu bado serikali haijaweza kuja na nishati mbadala inayopatikana ili wananchi waweze kuipata kwa urahisi na kwa bei nafuu kulingana na hali halisi ya uchumi wa wananchi ili sasa wananchi hao waweze kuhamasishwa kuachana na matumizi ya mkaa ili kuokoa misitu yetu.

**Mheshimiwa Spika,** tukumbuke ni serikali hii iliyowaaminisha wananchi kuwa tuna akiba kubwa ya gesi na hivyo gesi itapatikana kwenye kila

nyumba kwa bei nafuu sana jambo ambalo sio kweli hata kidogo. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inazo taarifa kuwa mpaka sasa bei ya gesi ni ghali  kwani mtungi ambao unaweza kutumiwa na familia yenye matumizi ya wastani ni gesi ya shilingi 50,000/- kwa mtungi wa kilo 15 tu kwa mwezi.

**Mheshimiwa Spika,** hivi karibuni Mkoani Dodoma serikali kupitia kwa Waziri wa Wizara hii ilitoa katazo la kusafirisha mkaa kutoka Wilaya moja kwenda nyingine na kunukuliwa na gazeti la Mwananchi la tarehe 11, April 2017 lenye kichwa cha habari ***"Mwisho Julai kusafirisha mkaa***" lilieleza kuwa mkaa utaruhusiwa kuchomwa na kuuzwa ndani ya Wilaya husika tu.

**Mheshimiwa Spika,** kauli hii sio tu imeshangaza umma lakini pia **inawagawa Watanzania**. Ni kauli ambayo isipoangaliwa kwa kina inaweza kuleta shida kwenye jamii.Tujiulize, wananchi wanaoishi Wilaya za mijini au katika ya majiji wao watachoma vipi mkaa na watachomea wapi? **Mheshimiwa Spika,** mpaka sasa ni Watanzania wachache wenye uelewa wa kutosha kuhusiana na makaa ya mawe. Ni ukweli usiopingika wapo Watanzania wengi ambao hawajawahi kuona makaa ya mawe.Japokuwa serikali imetoa kauli ndani ya Bunge hili kupitia Wizara ya nishati na Madini tarehe 18 Mwezi, 2017 kuwa serikali ina hazina kubwa ya makaa ya mawe ila ukweli ni kuwa makaa ya mawe yanakayochimbwa nchini yanatumika zaidi katika shughuli za uzalishaji viwandani kuliko majumbani. Vyombo vinavyotumiwa kwa matumizi ya kupikia na Watanzania walio wengi ni vyombo ambavyo haviwezi kuhimili moto wa makaa ya mawe.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kufanya utafiti wa kina kuhusiana na matumizi ya makaa ya mawe

majumbani kwani nchi nyingi duniani hutumia makaa haya kwa ajili ya matumizi ya viwandani tu.Je, athari zake kiafya ni zipi hasa kwa watakao tumia kwa ajili ya kuchoma nyama, mahindi na vyakula vingine vinavyohitaji moto wa moja kwa moja (direct heat).

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kuwa vyombo mbalimbali vya habari wakiwemo viongozi wa serikali wenye mamlaka na suala hili kulizungumzia hadharani suala la kukataza matumizi ya mkaa jambo la kushangaza ni kuwa mnamo tarehe 19/05/2017 katika mitandao mbalimbali ya kijamii ilisambaa taarifa kwa umma kutoka kitengo cha Habari na Mawasilino kwa Umma cha Wakala wa Huduma za Misitu (TFS) likipinga kauli iliyotolewa kuhusiana na katazo la usafirishaji na matumizi ya mkaa. Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kujua kama kweli taarifa hiyo ilitoka katika kitengo hicho kwani mnamo tarehe 10 April 2017 Mheshimiwa Waziri tayari alikuwa ametoa taarifa rasmi kwa umma katika mkutano wa 24 wa Baraza la Wafanyaakazi katika sekta ya maliasili na utallii katika ukumbi wa LAPF-Dodoma. Serikali ituambie kauli rasmi ya serikali kuhusiana na matumizi ya mkaa ni ipi?

## 5.2 UFUGAJI WA NYUKI

**Mheshimiwa Spika,** kazi ya ufugaji wa nyuki ni kazi ambayo imeweza kuwasaidia Watanzania wengi kunyayua kipato chao hususani miaka ya hivi karibuni. Hii ni kutokana na wengi kujitahidi kutafuta njia za kuanza kufuga nyuki kwa njia ya kisasa ziadi.

**Mheshimiwa Spika**, bado kuna changamoto nyingi katika sekta ya ufugaji wa nyuki kutokana kukosekana kwa masoko ya uhakika, serikali kutokuchukua jitihada za makusudi za kutangaza asali inayotoka Tanzania katika masoko ya kimataifa, na zaidi serikali kutokutenga bajeti ya kutosha hasa katika kukamilisha mapitio ya Sera ya Taifa ya

Nyuki. Mpaka sasa mapitio ya Sera hii yameshindwa kukamilika kutokana na uhaba wa fedha.

**Mheshimiwa Spika**, jambo hili linashangaza sana. Tukumbuke kuwa serikali ya Chama cha Mapinduzi kupitia Waziri Mkuu aliyepita ilijipambanua kwa ufugaji bora wa nyuki lakini jitihada zile alizozionyesha Waziri Mkuu aliyepita ni sawa ameondoka na jitihada zile. Hii ni kutokana na serikali ya sasa kutojali sekta ya ufugaji wa nyuki. Jambo hili linatia mashaka kwani inaonekana kila kiongozi anakuja na jambo lake la kipaumbele na pale anapoondoka jitihada zake nazo zinatupwa kapuni. Ni vyema serikali itambue serikali ni taasisi na sio mtu hata akiondoka yale mazuri yanayofanywa yapaswa kuendelezwa.

**Mheshimiwa Spika,** ili kuthibitisha jambo hili kwa mujibu wa Randama ya Wizara Jedwali namba 9,ukurasa wa 68 serikali imetenga shilingi milioni 200 tu kutoka vyanzo vya ndani tena kwa ajili ya kujenga uwezo. Huku fedha nyingine zikitegemea wahisani kutoka Norway, Belgium na Finland. Yaani bajeti ya sekta ya misitu na nyuki ni bajeti ya wahisani tu.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kuangalia upya sekta hizi zinazochangia kukuza pato la familia na kutafuta namna bora zaidi ya kuwezesha sekta hizi kwani zinagusa moja kwa maisha ya Watanzania wengi. Mheshimiwa Spika, Uchumi wa viwanda utaweza kukua endapo uchumi huo utaweza kugusa maisha ya wananchi moja kwa moja. Hivyo basi, sekta hizi zipewe kipaumbele ukiwa ni pamoja na kuwa na viwanda vidogo vidogo vya kusaidia uhifadhi wa asali pamoja na ufungashaji wa asali unaoendana na viwango vya kimataifa (parkaging).

## 6.0 UCHAMBUZI WA BAJETI YA WIZARA

**Mheshimiwa Spika,** katika mapitio ya utekelezaji wa mpango wa maendeleo na bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017 fungu 69, jedwali namba 10 Wizara hii imetengewa jumla ya shilingi **51, 803, 284,000** tu kama fedha za maendeleo ambapo kati ya fedha hizo zilizotengwa **17,000,000,000** ni fedha za wahisani kutoka nje.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara hii ni wizara nyeti inayochangia sana fedha za kigeni. Ni Wizara inayotoa ajira na inachangia uchumi wa nchi . Kupewa fedha ndogo za maendeleo kiasi hicho maana yake ni kuwa shilingi ya Tanzania inakuwa katika hatari ya kuzidi kuporomoka. Mpaka sasa dola moja ya kimarekani (1 USD) **ni sawa na shilingi 2,239.01** ikilinganishwa na shilingi 2,144.27 mwaka 2015, na 2,170.44 mwaka 2016 kwa mujibu wa gazeti la Mtanzania la tarehe 4 April 2017.

**Mheshimiwa Spika,** serikali kuendelea kushindwa kuuza huduma za utalii nje ya nchi na vilevile kushindwa kuwasaidia wafanyabiashara katika sekta ya utalii na hoteli kwa kuhakikisha kuwa inakuwa na masharti nafuu katika usajili ili ikupunguza wingi wa kampuni bubu ambapo mpaka sasa kati ya kampuni 1,050 ni kampuni 300 tu ndio zilizokidhi vigezo vya usajili, kwa sababu hiyo ni wazi kuwa sekta hii haitaweza kuongeza tija kwenye uchumi wetu. Na pia kupunguza kodi zisizo za lazima kwa wafanyabiashara ili waweze kufanya kazi kwa ufanisi kwa kuzingatia vigezo vya kimataifa na kutoa huduma za kisasa ili kuvutia watalii wengi zaidi ni jambo litakaloisadia sekta hii kufanya vizuri zaidi balada ya kuendelea kuwa na bajeti tegemezi kutoka kwa nchi wahisani.

## 7.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** mpaka sasa sekta nyingi hazifanyi vizuri kutokana na mapato hafifu yanayokusanywa na serikali kwa hivi sasa hali inayopelekea hali mbaya ya uchumi wetu. Lakini pamoja na hilo sekta hii ya Maliasili na Utalii inaweza kuwa mkombozi katika kuchangia uchumi hususani miradi ya maendeleo endapo tu serikali itaamua kuweka kipaumbele kuhimiza uwekezaji kwenye sekta ya utalii kwani matokeo yake yanaweza kuwa makubwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upizani haitasita kuendelea kuishauri serikali kwa kuwa nchi hii ni yetu sote na endapo tutanyamaza basi ni hakika lori hili tulilolipanda linaweza kumshinda dereva na sote tukajikuta shimoni

**Mheshimiwa Spika,** hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka serikali kuja na majibu kwa maswali na hoja ilizohoji na pia kuufanyia kazi ushauri uliotolewa ili kujenga taifa lenye tija. Pale ambapo tutashindwa kusema kwa kushauri au kukosoa, basi tujue wazi kutakuwa tumeua taifa hili .Kuwanyima wenye akili mbadala kusema maana yake ni kuwalazimisha Watanzania kuwaza kwa namna inayofanana jambo ambalo litahatarisha amani ya nchi na ni ukiukwaji mkubwa wa utawala bora. Mwalimu Nyerere alisema maneno haya **"tuweke utamaduni wa kudhibiti viongozi wetu kama wanavunja sheria ya nchi, tusiogope! tukianza kuwa waoga, I promise you! Mtatawaliwa na dictators. I promise you!, ninyi wabunge mkiogopa ogopa na mkisema Mzee wanakuwa wakali I promise you, you will be under dictatorship"**. Kwa maneno haya yenye busara za hali ya juu za muasisi wa Taifa hili basi ijifunze kupokea maoni mbadala hata kama hayaifurahishi kwani kufanya hivyo kutaisaidia

nchi yetu na tutakuwa tunayaishi yale aliyoyasema Mwalimu Nyerere kwa vitendo.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema maneno hayo, naomba kuwasilisha.

…………………………………….

**ESTHER NICHOLAUS MATIKO (Mb)**

Msemaji Mkuu Kambi Rasmi ya Upinzani - Wizara ya Maliasili na Utalii

23 Mei 2017